
# Tulikuwa tumepoteaje?

Dhambi ni jambo lolote tunalofikiria, tunalosema au tunalo-fanya ambalo linaenda kinyume na mapenzi ya Mungu. Mwenyezi Mungu hapendi dhambi kwa kuwa dhambi zinawadhuru watu. Dhambi huleta huzuni, ugonjwa, ugomvi na kifo. Bibilia inasema kwamba watu wote duniani wanaten-da dhambi. Yaani, binadamu wote wameenda kinyume na upendo wa Mungu (Warumi 3;23) Dhambi zimetutenganisha na Mungu wetu. Gharama ya dhambi zetu ni kifo.

# Nani aliyetuokoa?



HABARI NJEMA ni kwamba Mungu ana-kupenda zaidi! Alimtuma mwanawe Yesu kukuokoa ili urudi kwake.

> **“Kwa maana Mungu aliupenda ulimwengu kiasi cha kumtoa Mwanae pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.”**
> (Yohana 3:16)


Yesu alikuwa binadamu na pia ni mwana wa Mungu. Alikuwa hana dhambi. Wakati alikufa msalabani, alilipa ushuru



WNHS QR Booklet Kiswahili 2026.indd 3 2026/08/13 11:17:23

wa dhambi zako.  Lakini, pingu za kifo hazikumfunga, Yesu alifufuka! Yesu alitoka kaburini na sasa tunaweza kuishi maisha yetu pamoja naye milele na milele! Pokea habari njema.

## Hutawahi kuishi peke yako kamwe!



Isitoshe, ulipompokea Yesu, alikupatia zawadi ya kipekee, alikupatia Roho Mtakatifu! Kuanzia sasa, Roho Mtakatifu anaishi moyoni mwako. Wewe ni mtu mpya kuanzia sasa! Roho Mtakatifu ni mchungaji na msaidizi wako. Unaweza kuongea naye wakati wowote kwa kuwa anatembea nawe wakati wote. Ni rafiki yako wa kipekee.

## Chaguo ni letu

Kumbuka, Yesu ndiye njia ***pekee*** ya kupata baraka na mapenzi ya Mungu! Yesu alisema

> **“Mimi ndimi njia  ya  kweli na uzima, Mtu haji  kwa  baba yangu Ila kwa njia ya Mimi.”** (Yohana 14:6)



WNHS QR Booklet Kiswahili 2026.indd 4 2026/08/13 11:17:23

Mungu hatulazimishi kumchagua au kuchagua maisha ya wokovu. Hataki tuwe kama roboti bila fikra. Mungu anataka urafiki nawe kwa maana anawapenda watu wote. Matumaini yake ni kuchaguliwa na watu wake. Ni jukumu la kila mtu kumchagua Yesu.

Tukichagua kumfuata Yesu, tunatubu dhambi zetu na kumwomba mwenyezi Mungu atusamehe. tunapata wokovu tukisema 'Yesu ni Bwana" na kuamini katika mioyo yetu ya kwamba Yesu alishinda kifo alipofufuka.

## Baba Yetu

Ulipokubali Yesu awe mfalme wa maisha yako, uliokolewa na kuwa mwana wa Mungu!

> **"Bali wote waliompokea, aliwapa uwezo wa kuwa wana wa Mungu."**
> (Yohana 1:12)

Wewe ni mwana wa Yesu!
Sema kwa sauti:

**"MIMI NI MWANA WA YESU!"**

NDIO! Umekuwa mpya kuanza leo!
Sema kwa sauti:

**"MIMI NI MTU MPYA!"**



WNHS QR Booklet Kiswahili 2026.indd 5 2026/08/13 11:17:23

# ... ni nini kinachofuata?

Sasa, umekuwa mmoja wa familia ya Mungu. Wewe ni mwana wa Mungu, leo, na milele! Inamaanisha unauwezo wa kuongea na Mungu kila wakati. Tendo la kuongea na Mungu ni Kuomba au Sala. Ukiomba katika jina la Yesu, Mungu anapokea ombi lako na kukujibu vilivyo.

Mungu alitupatia kitabu cha maelezo yake — Bibilia takatifu! Bibilia ni njia moja ambayo Mungu anaweza kuwasiliana nasi. Kitabu hiki kina maelezo yote unayohitaji kumfuata Yesu. Ingekuwa vyema kuwa na Bibilia yako binafsi na kuisoma kila wakati. Mafunzo ya Bibilia yatakusaidia kuwa mtu bora kila siku.


Ni muhimu sana kutafuta Kanisa la Kikristo. Kanisa la Kristo na wafuasi au watu walioamua kumfuata Yesu. Hawa waumini watakuwa marafiki na wasaidizi wako katika safari yako ya wokovu.



WNHS QR Booklet Kiswahili 2026.indd 6 2026/08/13 11:17:23

# Chagua kunawiri!

Maisha yako ya wokovu ni kama mmea mbichi au mpya. Kila mmea unahitaji jua, maji na udongo ili kukua vyema. Bila vitu hivi mmea utakufa. Unahitaji mwangaza wa Bibilia. Unahitaji uhusiano wa karibu na Roho Mtakatifu. Unahitaji Kanisa la waumini wa Yesu. Sawa na mmea mpya, utakuwa na nguvu ya kiroho, utasimama wima na kumeremeta katika upendo wa Yesu!



# Uhusiano wako na Yesu utaimarika hivi:

1. **Omba.**
   Ongea na mwenyezi Mungu! Yeye ni rafiki yako wa karibu!





2. **Soma Bibilia.**
   Kumbuka huu ni mwangaza wako!



3. **Msifu Yesu!**
   Mshukuru Mungu kwa yote aliyofanya katika maisha yako.



4. **Jiunge na Kanisa la Waumini wa Yesu.**
   Pata nguvu katika maisha yako mapya na Yesu, pamoja na marafiki wanaompenda Yesu.



WNHS QR Booklet Kiswahili 2026.indd 8 2026/08/13 11:17:23

# HONGERA!

**Umechukua hatua ya muhimu kabisa katika maisha yako. Usisahau wewe ni mwana wa Mungu! Mungu anakupenda na ana mpango na wewe katika maisha yako!**

Andika jina lako hapa:

## YESU ANAKUPENDA

.............................................................. !

**Changanua kwa simu**



WNHS QR Booklet Kiswahili 2026.indd 9 2026/08/13 11:17:23